UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Kadhia ya Hijab nchini India kutoka kwa Mtazamo wa Kiislamu

**HABARI NA MAONI**
Vita vya Urusi na Ukraine ni Fursa ya Kurudi tena kwa Mlinzi na Ngao ya Kweli ya Kiulimwengu, Khilafah

**TOLEO JIPYA**
Ummah wa Kiislamu na Wanadamu Wote Wanahitaji Pakubwa Macheo ya Dola ya Khilafah

**JIBU LA SWALI**
Jambo Lisiloweza Kupatikana Lote, Haliachwi Lile Linalowezekana Kupatikana kwa Urahisi Kutokana Nalo



# Alhamdulillah! Hatimaye Wanachama Wetu Watatu Waachiwa Huru

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 04/1443 | Jumamosi, 25 Rajab 1443 H | 26/02/2022 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Alhamdulillah!
# Hatimaye Wanachama Wetu Watatu Waachiwa Huru

Hatimaye wanachama watatu wa Hizb ut Tahrir Tanzania, Ust. Ramadhan Moshi Kakoso (45), Waziri Mkaliaganda (37) na Omar Salum Bumbo(55) waliotekwa na kubambikiwa kesi ya ugaidi na kuwekwa kizuizini kwa miaka minne na nusu wameachiwa huru siku ya Jumatano tarehe 23 Februari 2022.

Siku rasmi ya kuachiwa kwao ilikuwa iwe tarehe 22 Februari, 2022 lakini kutokana na masharti yenye taklifu yaliyojitokeza yalipelekea kuchelewa kwa siku moja zaidi.

Katika kipindi chote walichokuwa kizuizini hawakupewa dhamana wala kesi yao kusikilizwa kwa kisingizio cha 'upelelezi unaendelea' na zaidi walinyimwa haki zao msingi kama kutembelewa na ndugu na kunyimwa nafasi ya kupelekewa chakula bora cha nje ya mahabusu.

Kuachiliwa kwao huru kumekuja baada ya miaka mingi ya kuwa kizuizini bila kesi yao kusikilizwa ambapo hatimaye Upande wa Mashtaka (DPP) umekiri kuwa hawana ushahidi wowote wa kuendelea na mashtaka husika dhidi yao.

Hizb ut Tahrir Tanzania, Waislamu kiujumla na wapenda haki wote wamefurahia kuachiwa huru (watatu hao) na kurudi kwa familia zao zilizokuwa zinawasubiri kwa hamu.

Katika hali hiyo, tunapenda kuwashukuru kwa dhati wote waliochangia na kushiriki katika kampeni rasmi na zisizo rasmi zilizopelekea kurejeshewa uhuru wao, shukrani hizi zikijumuisha baadhi ya Wanachuoni wa Kiislamu, Maustadhi, Maimamu wa misikiti na Waislamu kiujumla kwa dua zao na uungaji mkono wao. Pia tunashukuru baadhi ya vyombo vya habari, wanaharakati, wanasheria, wanasiasa nk. kwa kupaza sauti zao, rai na ushauri.

Tunasisitiza zaidi kuwa, kuachiwa huru kwa wanachama wetu watatu na kushindwa Upande wa Mashtaka kuleta ushahidi dhidi yao baada ya miaka minne na nusu ya kinachoitwa “uchunguzi” inaonesha wazi kuwa watatu hao hawana hatia kama ambavyo tumekuwa tukilisema hilo muda wote, kuwa watatu hao ni watu wanaojulikana kuwa wapenda amani na wanafamilia wanaojihusisha na Hizb ut Tahrir ambayo imeshikamana na njia isiyobadilika na ya wazi ya kuleta mabadiliko (ya Kiislamu) katika jamii iliyofuatwa na Mtume Muhammad (saw) inayojifunga kikamilifu na harakati zake kifikra na kisiasa tu bila ya kutumia nguvu au silaha.

Pia tunataka haki itendeke kwa wote waliowekwa kizuizini kwa dhulma, wawe Waislamu na wasiokuwa Waislamu, wapewe dhamana haraka iwezekanavyo au waachiwe huru.

Kwa kukhitimisha, tunarejea tena, hali ya kunajisi haki katika mfumo wa kikoloni wa kibepari ni tabia yake ya kimaumbile. Kwa hakika ni katika sharia za wahyi na chini ya kivuli cha dola ya Kiislamu ya Khilafah pekee kwa manhaj ya Utume ndipo uadilifu utakaposimama na kuangazia watu wote bila ya kuzingatia dini zao, rangi, matabaka, jinsia, kabila nk.

Na kauli yetu ya mwisho tunasema Alhamdullilah. Sifa zote njema na Shukran zote njema zinamstahikia Yeye Mwenyezi Mungu SWT.


**Masoud Msellem**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut Tahrir Tanzania**

Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

﴿ وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ
ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ
يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 27/1443 Jumatano, 20 Shaaban 1443 H 23/03/2022 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Kadhia ya Hijab nchini India kutoka kwa Mtazamo wa Kiislamu

Mnamo tarehe 15 Machi 2022, Mahakama Kuu ya Shirikisho ya jimbo la India la Karnataka ilitoa uamuzi, kwamba maagizo ya sare za shule ya mamlaka za vyuo (ambazo hazikuruhusu uvaaji wa Hijab/Khimar), hazikiuki uhuru wa kibinafsi au dini, ikikataa rufaa zote zilizowasilishwa na wanafunzi 9 wa kike wa Kiislamu wanaosoma katika Vyuo Vikuu vya Serikali za kutaka wavae Hijab na Khimar. Baraza la mahakama lenye wanachama 3 lilitaja zaidi kwamba Hijab haiwezi kuchukuliwa kama sehemu muhimu ya Uislamu, na hata kunukuu vifungu vya Quran ili kuwasilisha hukumu ya mahakama. Walalamishi tisa wameamua kupeleka kesi yao katika Mahakama ya Upeo ya taifa.

Uamuzi wa Mahakama Kuu unaotumia kurasa 129 umepata sifa mbaya kwa sababu mbalimbali. Uamuzi huo ulionyesha jaribio la Mahakama Kuu ya Karnataka inayoongozwa na serikali ya BJP kufafanua mipaka ya dini kwa wafuasi wake. Inaonekana kama utabikishaji mbaya wa mtihani wa umuhimu uliofafanuliwa na mahakama ya upeo ya nchi, ambapo ilitumia kwa mara ya kwanza mnamo 1954 kufafanua mahali ambapo sheria ya serikali itaupiku msimamo wa kidini. Ilikuwa tofauti kabisa na uamuzi mwingine wa Mahakama Kuu ya Shirikisho katika jimbo jirani la Kerala (pamoja na utawala wa jimbo lisilo la BJP), ambapo ilitoa uamuzi mwaka 2016 kuhusu kesi tofauti kwamba Hijab ni sehemu muhimu ya Uislamu. Inaonekana kama hatua nyingine kubwa ya chama tawala cha BJP kuwaridhisha Mabaniani wenye msimamo mkali na kuna uwezekano mkubwa wa kuenezwa katika taasisi na majimbo mengine ya India katika siku zijazo. Ulishuhudia sherehe za kitaifa za wafuasi wa itikadi kali wa Kibaniani, wakiwemo viongozi wa BJP, ambao msimamo wao ulikuwa chuki ya wazi kwa Hijab katika Uislamu kiasi cha kuwakatisha tamaa Waislamu nchini India na duniani, wanaotaka kutekeleza uvaaji wa Hijab katika Uislamu kama faradhi.

Lakini hukmu hii isiwashangaze Waislamu nchini India na duniani kote. Ni moja ya mizunguko ya mzozo wa kiulimwengu kati ya Uislamu na Ukafiri. Dhihirisho la mzozo huu sio tu katika mataifa 'yanayoonyesha' aina tofauti za Demokrasia, lakini pia katika ulimwengu wa Kiislamu ambao una aina zake tofauti za demokrasia, ikiwa sio udikteta. Tutaangalia mitazamo michache juu ya jambo hili ambalo ni muhimu sana kwa kila Muislamu.

1. Hijab na Khimar ni faradhi kwa Waumini wanawake (baada ya kubaleghe), iliyothibiti katika Quran na Sunnah, hivyo kukosa kushikamana nayo ni kuasi amri ya Mwenyezi Mungu (swt). Ni lazima itetewe kama amri ya Mwenyezi Mungu (swt) kwa wanawake, na kwa hakika ni utetezi sahihi. Mwelekeo wa kuitetea kama 'dhihirisho la uhuru' ni mbaya na ni lazima uepukwe, licha ya nia na matokeo yanayokusudiwa. Waislamu wanapaswa kutambua kwamba kutekeleza faradhi hii hakuathiriwi na uamuzi wowote wa mahakama kwani hakika haina hadhi mbele ya Mwenyezi Mungu (swt); badala yake, Waislamu lazima wajifunge kikamilifu faradhi hii.

2. Waislamu wanapaswa kutambua madai ya uongo ya nchi za Kidemokrasia za ulimwengu. Demokrasia kwa mujibu wa 'Usekula' inadai kulinda dini. Hata hivyo, maadili yanayodaiwa kuwa ya kisekula yanagongana kwa nguvu sana na matakwa ya kutabikisha Shariah ya Mwenyezi Mungu (swt) katika maisha ya umma kama vile kuharamisha pombe, kamari, zina, Riba na mengineyo - hata kama matakwa hayo yapo katika ardhi za Kiislamu. Demokrasia inataka kwamba maagizo na marufuku ya sheria kwa watu, yaamuliwe katika chombo cha utunzi wa sheria kilichochaguliwa bila kujali amri ya Mwenyezi Mungu (swt). Watu wa ardhi zisizokuwa za Kiislamu wanaendelea kupoteza imani na Demokrasia kwa unyanyasaji na ufisadi uliokithiri wanaoushuhudia na mmomonyoko wa haki na riziki zao. Waislamu wanapaswa kutambua kwamba utabikishaji wa Shariah ya Mwenyezi Mungu (swt) pamoja na hisia ya juu ya uwajibikaji na ikhlasi utaleta amani na ustawi wa dunia.

3. Waislamu wanapaswa kutambua kwamba nchi za Kidemokrasia, Kijamhuri, Kidikteta, Kifalme hutunga sheria ambazo ni za kiholela, zinazobadilika kulingana na wakati, ambazo huridhisha wingi wa kura kama malipo ya

*Endelea... UK 4*

kuchaguliwa, zinazowatuza washawishi waliofadhili uchaguzi wa madaraka yao, ambayo hushibisha tamaa zao mwenyewe. Zaidi ya hayo, mahakama inayodhaniwa kuwa huru inaweza kutoa uamuzi tofauti kwa dhurufu zile zile kiholela na kwa ubaguzi. Kwa mfano, vifungu ndani ya Katiba ya India Kifungu cha 370 kinachohusiana na haki maalum za Kashmir kilitumiwa na mahakama ili kuunga mkono wakati wa enzi ya chama cha Congress, lakini ikavipiga marufuku wakati wa enzi ya chama cha BJP. Bila kusahau unyanyasaji na ufisadi unaotokana na kutojali kuhesabiwa Siku ya Kiyama na Mwenyezi Mungu (swt), ambapo mtawala wa watu ndiye mwenye hesabu kubwa. Ambapo katika Uislamu Shariah ya Mwenyezi Mungu (swt) inayotolewa na dalili za kina ndani ya Quran na Sunnah ndio msingi wa sheria, ina kanuni za fiqh za kuvua utekelezaji maalum wa sheria hizo ambao inafaa kwa kila zama na mahali, inayotazamwa kama uaminifu mkubwa juu ya watu na kutahadharishwa kwa kiwango cha juu cha kuhesabiwa Siku ya Kiyama ili kujiepusha na unyanyasaji na ufisadi.

4. Waislamu wanapaswa kutambua kwamba sheria nyingi na maamuzi ya mahakama yanazofanyika sehemu mbalimbali za dunia, kama vile India, Palestina, Tunisia, Jordan, Uingereza, Ufaransa, Marekani (na kwengineko) zinaafikiana na maagizo ya Umoja wa Mataifa ya CEDAW ambayo yanaangalia kwa chuki dhidi ya utekelezaji Shariah ya Mwenyezi Mungu (swt) kwa ajili ya wanadamu, wakati huo huo inashajiisha sheria zilizokatazwa na Mwenyezi Mungu (swt). Hivyo ndivyo hali ilivyo kuhusiana na mirathi, ndoa, talaka, hijab na mengineyo. Msimamo mbaya unaoonyeshwa na serikali kote duniani ni uwakilishi wa wazi wa utawala wa Kimagharibi (au Urasilimali) wa ulimwengu unaouweka ‘uliberali’ (wa aina zote) juu ya Shariah ya Mwenyezi Mungu (swt) chini ya pazia la ‘Usekula’. Sio tu kuathiri Uislamu na utendaji wake bali ni tishio kwa dini zote, lenye thamani ya dhati.

5. Waislamu wanapaswa kutambua kwamba tangu kuvunjwa kwa Khilafah, mnamo tarehe 28 Rajab 1342 H (miaka 101 Hijria iliyopita), ulimwengu ulipoteza utawala (hukm) wa Mwenyezi Mungu (swt) duniani, Umma wa Kiislamu ulipoteza ngao yake. Fauka ya hayo, mfumo wa utawala wa Khilafah unadhamini utekelezaji wa imani za kidini kwa Dhimmi (wasiokuwa Waislamu ndani ya dola ya Khilafah) kama jambo lililowekwa ndani ya Shariah. Na iwapo Shariah ya Mwenyezi Mungu (swt) itatishiwa na wajinga miongoni mwa wanadamu, Dola ya Khilafah inatarajiwa kutoacha kutumia gharama yoyote, majeshi na silaha ili kuondoa vitisho hivyo.

Hizb ut Tahrir inawausia na kuwatahadharisha watawala wa India na ulimwengu. Kuweni na busara katika vitendo vyenu kuhusiana na mambo ya Waislamu. Kuregea kwa mfumo wa utawala wa Khilafah kumekaribia kama ilivyothibitishwa na hadith ya Mtume (saw). Tunathibitisha kujitolea kwetu kuhesabu kila ukiukaji wa Shariah ya Mwenyezi Mungu (swt). Ama kuhusu kuhesabuwa na Mwenyezi Mungu (swt) Siku ya Kiyama, ni jambo la yakini madhubuti lililo dhahiri mithili ya mwangaza wa mchana.

(وَسَيَعْلَمُ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَيَّ مُنْقَلَبٍ يَنْقَلِبُونَ)

**“Na wanao dhulumu watakuja jua mgeuko gani watakao geuka.”** [Al-Shu'araa: 226]

**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Vita vya Urusi na Ukraine ni Fursa ya Kurudi tena kwa Mlinzi na Ngao ya Kweli ya Kiulimwengu, Khilafah

**Habari:**

Mnamo Alhamisi, 24 Februari 2022 Urusi iliivamia rasmi Ukraine na hivi sasa wamo katika vita vikali. Vita hivi ni kupamba moto kwa mzozo baina ya Urusi na Ukraine ulioanza tokea mwaka 2014 kutokana na kubadilishwa kwa uongozi wa Kiev. Hapo awali uongozi ulikuwa unaegemea Urusi na baadaye ulipinduliwa na sehemu yake kuchukuliwa na uongozi unaoegemea Magharibi (Amerika na NATO).

**Maoni:**

Mzozo huu mpya unafichua kwa mara nyingine uhadaifu wa ile inayoitwa dola kuu duniani, Amerika katika mahusiano yake na mataifa mengine. Amerika chini ya utawala wa Obama ilizitumia asasi za kijeshi za mauaji za Urusi katika kusambaratisha mapinduzi ya kweli nchini Syria. Utawala wa Trump ukayatishia mataifa ya Ulaya (NATO) ili kuongeza maradufu michango yao ya kifedha kwa ajili ya kulindwa dhidi ya vitisho vya Urusi. Na mtawalia, utawala wa Biden umeanzisha vita huko Ulaya kwa kuichochea na kuisukuma Urusi kuivamia Ukraine kijeshi na hatimaye kutishia usalama wa Ulaya yote. Kwa kuongezea, imetangaza vikwazo kwa Urusi.

Urusi ina maradhi ya ukubwa kutokana na historia yake ya zamani kama mshikadau mkuu wakati ilipokuwa ndio kiongozi wa Muungano wa Jamhuri za Kijamaa za Kisoviet (USSR) kabla kuanguka kwake mnamo 1991 kupitia mikono hiyo hiyo ya Amerika kupitia vita vya uwakala. Hivyo basi, inaghurika na mbinu za Amerika na kujipata kuwa inatekeleza makosa ya kisiasa ambayo huisababishia madhara makubwa. Urusi na Ukraine zote zinatumika kama vikaragosi vya kisiasa na utawala wa Kiamerika ili kuweza kuitathmini upya sera yake ya kigeni katika kujitayarisha kupambana na kuchipuza kwa ushindani wa Uchina dhidi ya uchumi wa Amerika na mshikadau yeyote anayemuunga mkono Uchina.

Ni wazi kwa kuzingatia yaliyoko hapo juu kwamba Amerika inatanua katika mbinu hadaifu za kisiasa. Fauka ya hayo, mataifa yote ya kirasilimali ya kisekula yameasisiwa juu ya msingi sawa wa kupima vitendo kwa kuzingatia manufaa na maslahi. Kwa hiyo, haishangazi kushuhudia Urusi ikiivamia Ukraine, Amerika ikiivamia Iraq n.k kwa kutumia visingizio vyovyote ambavyo vitawapelekea kufikia lengo kwa kuwa lengo huhalalisha njia. Bila shaka mikono ya utawala wa Amerika inatona damu za Waukraine, kwa sababu wao ndio mabwana katika kupanga njama katika mzozo wote huo! Hivyo basi, wao ni washirika katika uhalifu pamoja na utawala wa Urusi.

Ama kuhusiana na vilio vya kiulimwengu ni thibitisho jingine kwamba kiuhakika mfumo wa kirasilimali wa kisekula umefeli kupindukia katika kuwasimamia wanadamu. Ndio tunashuhudia majanga yasiyohesabika kama natija ya uchochezi wa vita usioingia akilini kutoka kwa inayodaiwa kuwa ni mlinzi wa amani duniani. Mizozo ya kuendelea inatokomeza Somalia, Kashmir, Syria, Libya, Xinjiang, Uzbekistan, Afghanistan n.k. Hili limepelekea mwito wa kutaka mlinzi na ngao ya kweli mbadala dhidi ya vita fisidifu ambavyo SIO kwa ajili ya kumridhisha Mwenyezi Mungu (swt). Sasa ni fura ya kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume. Fursa adhimu ya kuwakomboa wanadamu kutoka katika minyororo ya Ukafiri hadi kwenye nuru ya Uislamu.

Khilafah haitokuwa tu mdhamini wa kweli wa amani, bali pia itajituma kurudisha mpangilio na ustawi ambao hivi sasa unakosekana chini ya zama hii ya mfumo wa kirasilimali wa kisekula. Zama ambayo pengo la ukosefu wa haki unaendelea kukua kwa kasi inayoshtusha. Ambapo sera za walio nacho na wasiokuwa nacho imemakinishwa kwa kina na inaendelea kupatilizwa na kipote cha wachache walioko katika kilele cha uongozi kama inavyoshuhudiwa leo nchini Kenya na ulimwenguni kwa ujumla. Kutaabika kwa watu ni fursa ya kibiashara kwa tai wa kiuchumi wanaoghilibu kuwa ni wajasiriamali kama ilivyofichuliwa na Covid-19, janga la kimakusudi lililopangwa!

Muda wa Khilafah uko nasi baada ya miaka 101 (Hijria) ya kutokuwepo. Hii ni fursa ya dhahabu kwa yeyote anayefanya kazi kwa bidi ya kurudi kwake, akiwa na matumaini na kuomba kheri, amani, usalama na ustawi duniani. Kurudi kwake ndio mwokozi pekee kutoka katika michafuko hii ya kujirudia. Wakati wa kuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu (swt) ni sasa:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسۡتَجِيبُواْ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمۡ لِمَا يُحۡيِيكُمۡۖ

**“Enyio mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele.”** [Al-Anfal 8: 24].

**#أقيموا_الخلافة #الخلافة_101**
**#TurudisheniKhilafah #YenidenHilafet**

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Ofisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

 Email: info@uqab.or.ke

Hotuba katika Msikiti wa Al-Aqsa Uliobarikiwa

# Ummah wa Kiislamu na Wanadamu Wote Wanahitaji Pakubwa Macheo ya Dola ya Khilafah



Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu (swt) aliyesema:

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ

**“Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watapo simama Mashahidi”** [Ghafir: 51].

Na rehema na amani zimshukie yule ambaye Mwenyezi Mungu amemtuma katika safari ya Israa kutoka Msikiti wa Al-Haram hadi Al-Aqsa iliyobarikiwa.

**Enyi Waislamu...** Enyi watu wetu katika viunga vya Msikiti wa Al-Aqsa na Ardhi Iliyobarikiwa... Enyi Ummah wetu kipenzi katika sehemu zote za dunia:

Tunasimama mbele yenu leo katika Masra ya Mtume wenu Mtukufu, katika kumbukumbu ya mwaka wa 101 wa kuvunjwa kwa Dola ya Kiislamu ya Khilafah. Tunasimama kwa mara nyingine tena huku kila mmoja akikabiliwa na maafa yaliyoupata Umma wa Kiislamu kwa sababu ya kuvunjwa Khilafah... janga lililowapata watu wa Palestina hasa huku wakiendelea kugeuza makaa ya moto kutokana na athari za kukosekana kwa Khalifa, ngao ambayo Waislamu hupigana nyuma yake, na hujihami kwayo. Wakafukuzwa katika ardhi yao baada ya kunyakuliwa. Tunawatazama wakiua asubuhi na jioni kwenye televisheni, wakitishiwa na walowezi katika vitongoji na miji, wanaochafua Msikiti wa Al-Aqsa ili kutekeleza ibada zao humo. Watu wa Ghaza bado wanateseka chini ya mzingiro mkali wa dhulma, yote haya yakiwa kwa ushirikiano wa watawala wa Kiislamu, ambao wanakimbia kuelekea kwenye uratibu, usawazishaji mahusiano na usaliti kwa namna ya wazi bila ya kumuogopa Mwenyezi Mungu au kuwaonea haya waja Wake.

**Enyi Waislamu:** Ummah mzima unaishi katika maafa ya kuvunjwa Khilafah... Unaishi katika maafa hayo huko Ash-Sham, ambapo watoto na wanawake wake waliuawa mbele ya wanaume wake, miji yake ikavunjwa na watu wake kuwa wakimbizi. Watu wa Iraq na Afghanistan wanaishi ndani yake, wanateseka kutokana na matokeo ya vita vilivyopiganwa dhidi yao na wakoloni, ambao waliteketeza kila kitu na kuharibu maeneo ya mijini katika vita vilivyotangazwa dhidi ya Umma wa Kiislamu. Athari za kuvunjwa kwa Khilafah ziliwaathiri watoto wa Kiislamu waliotawanywa kote ulimwenguni kutokana na dhulma na ukandamizaji. Watoto wa Kiislamu wanatekwa nyara kutoka kwa familia zao nchini Uswidi na kwingineko ili kuwekwa pamoja na familia za Kikristo zitakazowatenga na dini yao!

Waabudu ng'ombe walitushambulia, na wakavua hijab kutoka kwa vichwa vya wanawake wetu, ambao ni wanyonge na wasio na msaada na hakuna wa kukemea hili! China inaendelea kuwaua Waislamu wa Uyghur, kuwakandamiza na kuwazuia kufanya ibada, kama ilivyo kwa Myanmar.

**Enyi Waislamu:** Tawala za vibaraka alizoziunda mkoloni katika nchi yetu baada ya kuvunjwa Khilafah yetu na kugawanywa kwa Ardhi yetu ndio vinara katika vita vyake dhidi ya Umma wa Kiislamu. Wanakandamiza watu, wanarusha makombora vichwani mwa watu, wanawatupa wanazuoni wanyofu gerezani, na wanawasilisha utajiri wa nchi kwenye sahani ya fedha kwa wakoloni wa Magharibi. Wanapigana vita

*Endelea... UK 7*

dhidi ya Dini, thaqafa na imani ya Ummah katika vyombo vya habari na mitaala ya kielimu, wakiondoa kile kilichosalia cha harufu nzuri ya Uislamu kwenye mitaala na kutia saini mikataba ya kimataifa kama vile CEDAW iliyolaaniwa ili kuyatekeleza kwa Waislamu ili kuwatenganisha zaidi na Dini yao.

Hii ndiyo hali yenu baada ya miaka mia moja na moja baada ya kuvunjwa Khilafah mithili ya mayatima kwenye karamu za waovu, damu yenu, heshima yenu, mali yenu na matukufu yenu vinajuzishwa kukiukwa.

**Enyi Watu:** Leo tumesimama katika Msikiti wa Al-Aqsa na dunia nzima inateseka kwa sababu ya kutokuwepo Uislamu. Kwa sababu ya kukosekana kwa Khilafah kama dola ya kimataifa, watu walikoloniwa na utajiri wa nchi dhaifu ukaporwa, na dunia nzima imekuwa mateka wa maamuzi ya kihalifu ya Marekani na Urusi. Kwa sababu ya kutokuwepo Khilafah kama dola ya kimataifa, ulimwengu ulishuhudia vita viwili angamivu vya dunia, na hivi sasa wako ukingoni mwa vita vya tatu vya dunia, na ikiwa Ummah wa Kiislamu hautachukua hatua ya kuokoa wanadamu, ulimwengu huu utabaki kutawaliwa na matamanio ya marais wajinga na mizozo haribifu ya kimataifa.

**Enyi Watu:** Kutoka Msikiti wa Al-Aqsa, tunauhutubia Ummah wa Kiislamu hasa na watu wa dunia nzima kwa jumla, na tunawaambia Waislamu: Nyinyi ndio mnaoweza kuunusuru ulimwengu na wanadamu kutokana na dhulma ya mabepari na uhalifu wao. Nyinyi ndio wabebaji wa rehma na uongofu. Nyinyi ni mashahidi wa Mwenyezi Mungu kwa watu, basi je, mtatikisa vumbi kutoka mabegani mwenu na kuinuka pamoja utukufu wa Uislamu?

**Tunawaambia majeshi ya Kiislamu:** Nyinyi ni nguvu na ulinzi wa Waislamu, na kwa mikono yenu ufunguzi na ushindi hutokea. Mpaka lini mtabaki kuwa mateka wa tawala hizi vibaraka, zilizoua ndani yenu msukumo wa Jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu (swt)? Ni lini mtaghadhibika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (swt) na kuwapindua wasaliti hawa wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake (saw)? Je! wakati haujawadia kwa nyoyo zenu kujisalimisha kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na yale yaliyoteremshwa kwa haki, na kumnusuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kutoa Nusra kwa Hizb ut-Tahrir na Amiri wake, na kutoa ahadi ya utiifu (bay'ah) kwake mithili ahadi ya utiifu ya Answar, ambayo kwayo mnasimamisha Dini na kuibeba kama ujumbe wa kheri na mwongozo kwa walimwengu?

**Ama kwa watu wa dunia tunawaambia:** Urasilimali umevipofusha vyama na marais wenu, na moja ya uhalifu wao mkubwa ni kuchochea uadui dhidi ya Uislamu, licha ya kuwa ni rehema itakayokuokoeni, na kwa sababu ya kiburi chao na ubinafsi wao, hatma yenu imetishiwa na kutoweka. Yanayotokea Ukraine leo ni onyo ambalo linakutishieni endapo hamtawakomesha wahalifu hawa. Mabepari na viongozi wa nchi kuu hawapatii uzito isipokuwa kwa maslahi yao, nao ni uovu unaowasibu wanadamu. Na msipokimbilia kurekebisha mambo yenu, mtaathirika na zaidi ya yale yaliyokupateni katika vita viwili vya dunia.

**Enyi Watu:** Dunia nzima inahitaji nguvu mpya ya kimataifa ili kuupindua mfumo huu wa kihalifu, inahitaji Uislamu na Dola ya Khilafah, ili kuinusuru na jinai za nchi kubwa - Marekani, Urusi, Uingereza, Ufaransa na China - kwani jinai zao dhidi wanadamu ni za aibu. Dola ya Khilafah ni mwokozi wa wanadamu na itabadilisha mahusiano ya kimataifa na kuyaunda tena, ni kimbilio la wanyonge katika ulimwengu mzima.

Ni Dola kwa njia ya Utume, inatawala kwa sheria ya Mwingi wa Rehma, ambamo uadilifu huthibitika na wema huenea, wanaodhulumiwa wanatendewa uadilifu, dhalimu anahisabiwa, na anasukumwa juu ya haki.

**Ni Khilafah kwa njia ya Utume** ambapo watu wote humiminika kwake, kwa sababu ndio wokovu wao, ngome yao, ngao yao. Twamuomba Mwenyezi Mungu (swt) ayafanye macheo yake yawe karibu, ni wakati sasa wa Dini yetu kudhihiri na bendera ya Mtume wetu kunyanyuliwa. Huu ndio wito wetu kwenu, ndani yake kuna uhai na wokovu wenu.

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ**

**"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa"** [Al-Anfal: 24]

Ewe Mwenyezi Mungu, tunakuomba Khilafah Rashida kwa njia ya Utume ambayo kwayo tunamridhisha Mola wetu Mlezi na kuregesha utukufu na heshima yetu, kwayo tunaikomboa ardhi yetu na njia ya Mtume wetu.

Ewe Mwenyezi Mungu zifungue nyoyo za watu wenye nguvu na ulinzi ili wainusuru Dini yako na kuisimamisha kama Khilafah Rashida kwa njia ya Utume.

Ewe Mwenyezi Mungu, inyanyue bendera ya Uislamu ipepee juu ya kuta za Bayt Al-Maqdis, na uzifanye sauti za Takbira za majeshi ya Khilafah zisikike kwenye pembe zake kwa Rehma Zako, Neema Zako, na Fadhili Zako Adhimu. Na rehma na amani zimshukie yule aliye tumwa kama rehma kwa watu, na sifa njema ni za Mola wa walimwengu wote.

**H. 1 Sha'aban 1443**
**M. : Ijumaa, 04 Machi 2022**

**Hizb-ut-Tahrir**
**Ardhi ya Baraka-Palestina**



Email: info@uqab.or.ke

# HABARI NA MAONI
# Mashambulizi ya Urusi kwa Wanawake na Watoto Yanaakisi Kanuni za Kinyama za Sheria za Kisekula



**Habari:**

Mnamo siku ya Alhamisi, tarehe 17 Machi 2022, vikosi vya anga vya Urusi vililipua ukumbi mmoja wa michezo katika mji wa Mariupol. Jumuiya ya kimataifa ilianzisha kulaani kitendo hicho kote duniani kwani iliripotiwa kuwa neno la Kirusi la "watoto" liliwekwa wazi nje ya jengo hilo. Wakati wa shambulizi hilo la bomu, mamia ya raia walisemekana kuwa wamejihifadhi katika jengo hilo, wengi wao wakiwa familia zenye watoto.

Petro Andriushchenko, mshauri wa meya wa jiji hilo, awali alisema wafanyikazi wa dharura walikuwa wakihangaika kulifikia jengo hilo kutokana na kushambuliwa kwa makombora kila mara.

**Maoni:**

Ukatili usiobagua wa serikali zinazolenga wanawake na watoto katika hali ya mapigano sio jambo geni katika siasa za magharibi. Umma bado una kumbukumbu za kihakika kabisa za "mshtuko na hofu" ya mvua ya mabomu ambayo yaliyomiminwa kwa watoto wasio na hatia wa Iraq chini ya maagizo ya Marekani. Wapiganaji wa Urusi ni watendaji wenye uzoefu wa mauaji ya watoto huku majeshi yao yakiwa na mazoezi mengi nchini Syria. Damu takatifu, isiyo na ulinzi ya watoto wachanga waliozaliwa ililengwa sana kwani wodi za uzazi ziliharibiwa na nguvu kamili ya chuki ya Putin kwa watu wasio Warusi.

Vita haviwezi kuchukuliwa kuwa sehemu salama kwa binadamu yeyote, hata hivyo sheria za Kiislamu zinatambua kwamba kanuni za mapambano kamwe hazivuki mipaka mitakatifu ya kuwadhuru wasiokuwa wapiganaji, yaani wanawake, watoto na wanyama. Mwenyezi Mungu (swt) asema kwa uwazi katika Aya ya Quran Surah Al-Maida aya ya 32;

مِنْ أَجْلِ ذَٰلِكَ كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَأَنَّمَا أَحْيَا النَّاسَ جَمِيعًا ۚ وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِنْهُمْ بَعْدَ ذَٰلِكَ فِي الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ

**“Kwa sababu ya hayo tuliwaandikia Wana wa Israili ya kwamba aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote. Na hakika waliwajia Mitume wetu na hoja zilizo wazi. Kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika nchi.”**

Katika mfano mtukufu wa Khalifa Abu-Bakr (ra), iliharamishwa kitendo cha mapigano ya kiholela, kauli yake maarufu ilitoa amri zifuatazo;

“Mnapokutana na maadui zenu vitani, fanyeni inavyowapasa Waislamu wema.... Mwenyezi Mungu akikupeni ushindi, basi msitumie vibaya faida zenu na jihadharini msichafue panga zenu kwa damu ya mwenye kujisalimisha, wala msiguse watoto, wanawake, na wasio na madhaifu, na wanaume pia, ambao mtawakuta miongoni maadui zenu."

Pia, “Mnapopita katika eneo la adui, msikate mitende, wala miti mingine ya matunda, wala msiharibu mazao ya nchi, msiharibu mashamba, msichome nyumba... Uharibifu wowote usiwepo bila ya haja.”

Inasemekana alikwenda mbali na kusema kwamba pindi majeshi ya Kiislamu yanapokosa chakula, wanapaswa kuchukua chakula tu kutoka kwa raia pekee katika eneo la adui cha kutosha kwa mlo mmoja.

Kutokana na dalili hizi tunaweza kuona kwamba ukatili wa sheria ya kisekula ndilo jambo la kihakika linalohusika na siasa za dunia na sio kuregea kwa uadilifu na usalama wa Khilafah.


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Imrana Mohammad**





**Email: info@uqab.or.ke**

**JIBU LA SWALI**

# Jambo Lisiloweza Kupatikana Lote, Haliachwi Lile Linalowezekana Kupatikana kwa Urahisi Kutokana Nalo

**Swali:**

Ewe Amir Wetu, Assalamu Alaikum Wa Rahmatullahi Wa Barakaatuh.

Mwenyezi Mungu awahifadhi, awachunge, na awafungulie kheri kupitia mikono yenu.

Ni upi usahihi wa huu msingi wa kisheria? Na je yafaa kuutumia kama dalili ya kutekeleza hukmu za kisheria polepole? [msingi wenyewe ni:

**"ما لا يدرك كله لا يترك ما تيسر منه"** "Jambo lisiloweza kupatikana lote, Haliachwi lile linalowezekana kupatikana kwa urahisi kutokana nalo." Mwenyezi Mungu awabariki.

**Jibu:**

**Wa Alaikum Salaam Wa Rahmatullahi Wa Barakaatuh.**

Kwanza: Mwenyezi Mungu akubariki kwa kutuombea dua zako nzuri, nasi twakuombea kheri.

Bila shaka, wauliza kuhusu mambo mawili:

**Kwanza:**

Ni upi usahihi wa msingi wa kisheria usemao: "Jambo lisiloweza kupatikana lote, Haliachwi lile linalowezekana kupatikana kwa urahisi kutokana nalo."

Na pilii: waulizia ikiwa yafaa kuutumia kama dalili ya kutekeleza hukmu za kisheria polepole?

Na jibu juu ya hayo ni kama ifuatavyo:

1- Ama kuhusu swali lako juu ya usahihi wa msingi huu **"Jambo lisiloweza kupatikana lote, Haliachwi lile linalowezekana kupatikana kwa urahisi kutokana nalo".** Huu msemo una matamshi mengi yanayokaribiana, yanayozunguka katika vitabu vya wanazuoni. Kama vile "lisilowezekana lote, haliachwi lote" ama "lisilowezekana lote hakiachwi kingi chake" ama "lisilowezekana lote, kichache chake hakiachwi" ama "lisilowezekana lote, kichache chake zaidi pia hakiachwi" ama "lisilowezekana lote, haliachwi baadhi yake" pamoja na kuongezea tamshi lilokuja kwenye swali lako: "jambo lisiloweza kupatikana lote, "lisilowezekana kupatika lote haliachwi lile linalowezekana"... na baadhi husema kuwa hiyo ni "mifano" au ni "misemo" na wengine wanaieleza kuwa ni "misingi ya kisheria"... bali ni kana kwamba imepita kwenye midomo ya baadhi ya watu wakiizingatia kuwa ni hadithi kutoka kwa Mtume (saw), jambo lilomfanya mwanahadith wa Sham katika zama zake ambaye ni Ismail bin Muhammad bin Abd al-Haadi al-Jirahi, al-Ajluni, ad-Dimashqiy, Abu al-Fidaa, aliyekufa mwaka 1162 H, [Jambo hilo lilimfanya mwanachuoni huyu] kuitaja katika kitabu chake cha "Kashfu al-Khafaa" na kisha akasema: "lisowezekana lote, haliachwi lote" msingi huu ina maana ya aya isemayo: ﴿فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ﴾ **"Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo"** [At-Taghaabun: 16] na hadithi isemayo «اتَّقِ اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتَ» **"Mtii Mwenyezi Mungu kadiri unavyoweza"**. Na hilo tamko ni Qaaidah (msingi) na wala sio hadith".

Ametaja msingi huu pia Ahmad bin Abdilkarim al-Ghazy, al-Amiri, alokufa mwaka 1143 H kwenye kitabu chake "Al-Jidul Hathith fii Bayani Maa Laisa bi Hadith" akasema: "lisowezekana lote, haliachwi lote" hii ni Qaidah na sio hadith, na ina maana ya aya ﴿فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ﴾ **"Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo"** [At-Taghaabun: 16]

2- Kutokana na uchunguzi wa kina kuhusu hilo jambo, imebainika kwamba huo msemo "lisowezekana lote, haliachwi lote" marejeo yake ni kwenye Qaidah ya kisheria isemayo: "jambo linalowezekana haliondoki kwa sababu ya lisowezekana" ikiwa na maana kwamba, hayo ni matamshi mengine ya hii Qaida. Na hii Qaida [iliyotangulia hivi punde] ni Qaidah ilotajwa ndani ya vitabu vya misingi ya kisheria pamoja na dalili zake. Kwa mfano: anasema As-Suyutwi kwenye kitabu chake "Al-Ashbaahu wa Nadhair" [Qaidah ya thalathini na nane: **"الْمَيْسُورُ لَا يَسْقُطُ بِالْمَعْسُورِ"** "Linalowezekana kupatikana kwa urahisi halipomoshwi na jambo lisiloweza kupatikana kwa urahisi". Amesema Ibn Subki: [nayo hii Qaidah ni kati ya misingi mashuhuri iliyotolewa kwenye neno lake Mtume (saw): **«إِذَا أَمَرْتُكُمْ بِأَمْرٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ»** yaani: **"Pindi ninapowaamrisha jambo lolote basi lifanyeni kwa kadri mnavyoweza"**. Na pia Zarkashi ameitaja hii Qaidah ndani ya kitabu chake "Al-Manthur fil Qawaaid" akasema: "Hii Qaidah isemayo: **lisowezekana lote, haliachwi lote"** yarudi kwenye Qaidah ya "uwezo" juu ya baadhi ya msingi]. Na kwa hakika, aliifafanua na kubainisha mipaka yake pale alipozungumzia kuhusu maudhui ya ***"kitu kinachowezekana baadhi, je ni lazima?"***

3- Wanazuoni wametolea dalili hii Qaidah **"الْمَيْسُورُ لَا يَسْقُطُ بِالْمَعْسُورِ"** "Linalowezekana kupatikana kwa urahisi halipomoshwi na jambo lisiloweza kupatikana kwa urahisi" na zengine zinazofanana nayo, au kwa maudhui ya ***"kitu kinachowezekana baadhi, je ni lazima?"***

***Endelea... UK 10***

[walizitolea dalili] kwa neno lake Mwenyezi Mungu (swt) aliposema:

﴿فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُم﴾ **"Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo"** [At-Taghaabun: 16] na kwa kauli yake Mtume (saw) aliposema: «إِذَا أَمَرْتُكُمْ بِأَمْرٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ» yaani... **“Pindi ninapowaamrisha jambo lolote basi lifanyeni kwa kadri mnavyoweza”** (imepokewa na Bukhari kwenye Sahih yake, kutoka kwa Abu Huraira r.a) na hizi qaida wamezitolea mifano mingi ya ufafanuzi ili kuweka wazi uhalisia wake. Ametaja [As-Suyutwi] katika kitabu “Al-Ashbaahu wa Nadhair” matawi yake mingi, na tutataja tu baadhi yake:

“Ikiwa mtu amekatwa baadhi ya viungo, itamlazimu [katika udhu] kuosha viungo vilivyobakia”. Pia: mtu mwenye uwezo wa kupata baadhi ya [nguo] ya kujistiri, atawajibika kujisitiri nayo kwa namna itakayowezekana. Pia: mwenye uwezo wa kusoma baadhi ya Suratul Fatiha, ni lazima aisome tu, hakuna ikhtilafu [kwa wanazuoni]... pia: lau mtu atashindwa kurukuu na kusujudu, na [hakushindwa] kusimama, basi ni wajibu kusimama, hilo halina ikhtilaaf kwetu... pia: mwenye kupata baadhi ya pishi kwenye Idd ul Fitri, inamlazimu kuitoa [hiyo hiyo] kulingana na kauli sahihi zaidi...”

4- Kutokana na kutafiti mifano waliotolea wanazuoni juu ya msingi huu usemao: **(الميسور لا يسقط بالمعسور)** "Linalowezekana kupatikana kwa urahisi halipomoshwi na jambo lisiloweza kupatikana kwa urahisi" na iliyofanana nao, inabainika kwamba wao wanakusudia kwa msingi huu kuwa, hukmu maalumu iliyoamrishwa kisheria, na mukallaf akawa hana uwezo wa kutekeleza baadhi yake [ima] kwa sababu ya kushindwa, au kwa sababu ya uzito wake, basi kutekeleza yaliyobakia katika kitendo kilichaomrishwa hakupomoki kwake. Bali ni lazima kwake kufanya anayoweza kutokana na hicho alichoamrishwa. Kwa sababu, mukallaf anatakiwa kisheria kutekeleza anachoweza kutokana na maamrisho, kulingana na matamshi ya Kitabu [Qur`an] na Sunnah

﴿فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُم﴾، **"Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo"** [At-Taghaabun: 16] na kauli yake Mtume (saw): “«إِذَا أَمَرْتُكُمْ بِأَمْرٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ» yaani... “Pindi ninapowaamrisha jambo lolote basi lifanyeni kulingana na mnavyoweza”. Kwa mfano: mwenye kuswali ni lazima asome Surat ul-Faatiha kamili katika kila rakaa, lakini mtu anaposilimu na akataka kuswali hali ya kuwa hajui kwenye Surat ul-Faatiha isipokuwa baadhi yake tu, je hapo ni wajib kwake katika swala yake asome aya anazozijua katika Surat ul-Faatiha? Ama aache kabisa [asisome chochote] kwa sababu hajui isipokuwa tu baadhi yake? Jibu juu ya hilo: kulingana na hii qaidah ni wajib kwake asome kiasi anachojua katika sa Surat ul-Faatiha, na haitoswihi kwake kuacha kuisoma. Kwa sababu ***“kinachowezekana*** - ambapo hapa ni kusoma aya anazozijua katika Surat ul-Faatiha - ***hakiachwi - kwa ajili ya - lile lisilowezekana”*** [hapa ni kusoma aya asizozijua katika Faatiha]... na kwa mfano: ni lazima mukallaf anapotawadha aoshe mikono yake miwili hadi kwenye visususku, lakini akiwa amekatwa kiganja, je ni lazima aoshe sehemu zengine za mikono yake? Ama uoshaji wa hizo sehemu zengine za mkono utaondoka, kwa kuwa yeye hawezi kuosha baadhi ya mkono [kiganja]? Na jibu juu ya hilo: kulingana na hii qaaidah ni lazima kwake kuosha sehemu ilobakia [***ndio “kinachowezekana***] hata kama kuosha kiganja haiwezekani [***kisichowezekana***] kwa sababu, ***“linalowezekana haliachwi -kwa ajili ya - lile lisilowezekana”.***.. kwa hiyo basi, bila shaka maudhui ya hii qaidah kwa wanazuoni ni “hukmu ya kisheria iliyoamrishwa, na ikawa mukallaf hawezi kutekeleza baadhi yake kwa sababu ya uzito, basi hilo halitamuondolea ulazima wa kutekeleza kile anachoweza kutokana na kitendo kinachotakiwa”...

5- Hakika, qaidah isemayo ***““linalowezekana haliachwi -kwa ajili ya - lile lisilowezekana”*** na mfano wake, ni misingi isiyodhibitika. Ndio ni sahihi katika baadhi ya hali na sio sahihi katika hali zengine. Kwa mfano: mtu asoweza kufunga baadhi ya siku katika mwezi wa Ramadhan, sio wajib kwake kujizuia baki ya siku na awe kana kwamba kafunga siku nzima, [eti] kwa hoja kuwa ***““linalowezekana haliachwi -kwa ajili ya - lile lisilowezekana”!*** bali ni afungue [swaum] na atalipa swaum ya siku iliyompita... na hivyo ndivyo inavyodhihirika kwamba hizi qaaidah hazidhibitiki, kwa hiyo zaweza kutumika katika baadhi ya hali tu na haziwezi kutumika katika hali zengine. Na ili kutumika kwake kunahitajika ijtihaad katika kutafiti uhalisia [wa hali] inayotakiwa kutumika hizo qaida, na kujua hukmu za kisheria zenye kuhusiana nayo... na hakika wanazuoni walitanabahi kwamba hizi qaidah hazidhibitiki:

a) Ametaja As-Suyutwi kwenye “Al-Ashbaahu wa Nadhair” haya yafuatayo: [“Tanbihi: kuna mambo kadhaa yanatoka nje ya hizi qaidah, miongoni mwayo: mwenye kumiliki baadhi ya mtumwa katika kafara hatoacha huru, bali atahamia kwenye badali, bila ya ikhtilaaf. Na imeelekezwa kwamba, kulazimisha kuacha huru baadhi ya mtumwa pamoja na kufunga miezi miwili, itakuwa ni kuweka pamoja badali na kilichobadilishiwa, na kufunga mwezi mmoja pamoja na kuacha huru nusu ya mtumwa, hapo kutakuwa na utekelezaji baadhi ya kafara na hilo haliwezekani, hasa kwa kuwa Mwenyezi Mungu (swt) amesema: **فَمَنْ لَمْ يَجِدْ “Na ambaye hakupata...”** [An-Nisa: 92]. Na mwenye kuwa na baadhi ya mtumwa huyo basi [anahisabiwa kuwa] hajapata mtumwa... na miongoni mwayo: mwenye kuweza kufunga baadhi ya siku na akashindwa na kufunga siku nzima, huyo si lazima kwake kujizuia...”]

b) Kadhalika Zarkashiy amebainisha hili jambo katika kitabu “Al-Manthur fil Qawaaid” akasema: “[na baadhi inalowezekana je, ni wajib? Kuna vigawanyo vinne:

**Kwanza:** kuna linalowajibika kwa kukatikiwa, kama vile

***Endelea... UK 11***



Email: info@uqab.or.ke

ikiwa mwenye kuswali aweza kusoma baadhi ya Faatiha, basi itamlazimu kwa kukatikiwa...

**Pili:** kuna linalowajibika kulingana na kauli sahihi zaidi... na lau kwenye mwili wake kuna majeraha yanayomzuia kueneza maji, basi kulingana na Madh-hab ni aoshe viungo vizima, na atayammam badala ya kiungo chenye jeraha...

**Tatu:** kuna lisilowajibika kwa kukatikiwa. Kama vile akipata baadhi ya mtumwa katika kafara inayompasa, basi hatolazimika kwa kukatikiwa, kwa sababu sheria kusudio lake ni kukamilisha uachaji huru kadri inavyowezekana... na ataendea badali yake...

**Nne:** na kuna yasiyowajibika kulingana na kauli sahihi zaidi. Kama vile lau mtu mwenye hadath [asiye na udhu] aliyekosa maji, akipata theluji au umande, na ikashindikana kuziyeyusha, basi hapo hatowajibika kupangusa kichwa nayo, kulingana na Madh-hab. Kwa sababu, mpangilio ni wajib, na haiwezekani kutumia hii [theluji] kwenye kichwa kabla ya kutayammam kwa ajili ya uso na mikono miwili..."]

Kwa hiyo, yadhihirika kwamba hiyo/hizo qaidah zilizoashiriwa sio sahihi moja kwa moja, wala sio makosa moja kwa moja. Bali huwa ni sahihi na zilonyooka katika baadhi ya sehemu, na haziwi sahihi katika sehemu zengine.

**Pili:**

Kuhusu kutumia hii qaidah **(ما يدرك كله لا يترك ما تيسر منه)** “Jambo lisiloweza kupatikana lote, Haliachwi lile linalowezekana kupatikana kwa urahisi kutokana nalo.” au **(الميسور لا يسقط بالمعسور)** "Linalowezekana kupatikana kwa urahisi halipomoshwi na jambo lisiloweza kupatikana kwa urahisi" kama dalili juu maudhui ya utabikishaji polepole wa hukmu za kisheria:

Bila shaka, kutumia hizi qaidah kama dalili ya kufaa kutabikisha polepole hukmu za kisheria, huko ni katika kuwahadaa watu, na katika kuizulia uongo dini ya Mwenyezi Mungu. Na hiyo ni kwa sababu, hakuna nafasi kabisa kutumia hizi qaaidah kama dalili ya kufaa kutekeleza sheria polepole. Na [nasema] hivyo kwa milango [hoja] nyingi:

1- Maana ya kutabikisha polepole hukmu za kisheria: ni kutekeleza sehemu kutokana na hukmu za kisheria katika baadhi ya mambo, na kutekeleza hukmu za ukafiri katika mambo mengine. Hilo ni kama vile: mikataba ya ndoa ifungwe kulingana na hukmu za Kiislamu, lakini riba, zinaa, unywaji pombe [hizi] ziruhusiwe! Adhabu ya mwizi ifanywe ni kukatwa mkono, lakini mzinifu na mlevi hawapewi adhabu...! Hivyo, itakuwa maana halisi ya ***“kutabikisha polepole hukmu za kisheria”*** ni kuhukumu kwa hukmu za ukafiri katika mambo maalumu badala ya kuhukumu kwa sharia. Na hili - bila shaka - liko mbali sana na maudhui ya qaidah **[ما يدرك كله لا يترك ما تيسر منه]** “Jambo lisiloweza kupatikana lote, Haliachwi lile linalowezekana kupatikana kwa urahisi kutokana nalo.” Kwa sababu, hii qaaidah yasema kwamba, kitendo ambacho kimeamrishwa na sheria ni lazima kitekelezwe baadhi yake kinachowezekana ikiwa baadhi nyengine sio rahisi kwa kukosekana uwezo. Kwa hiyo, qaaidah **haisemi** kwamba, yaruhusiwa kufanya haramu au kutekeleza ukafiri ikiwa hakuna uwezo wa kutekeleza uliyoamrishwa...!

2- Hizi qaidah zazungumzia kitendo kilicho **amrishwa** wala sio kitendo kilicho **katazwa.** Kwani kitendo kilichoamrishwa ni “kutekeleza sheria” ama kutekeleza isiyokuwa sheria bila shaka ni “jambo lilokatazwa” bali hilo miongoni mwa madhambi makubwa zaidi! Sasa vipi hizi qaaidah zitumiwe kama dalili juu ya kufaa kutekeleza hukmu za ukafiri?! Hivi hili si ni jambo la ajabu?!

3- Hakika wenye msimamo wa **tadarruj** wanakusudia kwa hilo: mtawala kutekeleza sheria polepole, na mtawala hakuna kitu kinachomzuia kutekeleza sheria, hivyo haitokuwa na nafasi hapa maudhui ya kutokuwa na uwezo, kwa sababu yeye ndiye mtawala! Kwa mfano: kitu gani kinamzuia mtawala Muislamu kutekeleza hukmu zote za kisheria badala ya kutekeleza hukmu za ukafiri kwenye sehemu nyingi za nyanja za maisha? Kwani yeye si ndiye mtawala hakika wa nchi?! Basi kwa nini hatabikishi hukmu za sheria? Bali hutanguliza hukmu za ukafiri?! Je, uhalisia wa mtawala ni mfano wa mtu asiyeweza kusimama katika swala kwa sababu ya maradhi aliyo nayo? Ikawa ulazima wa kusimama umeondoka kwake, na akaswali bila ya kusimama?! Zafanana kivipi hizi hali?

4- Na kabla ya yote hayo na baada yake, hakika nususi za kisheria zilizotumiwa kuwa dalili ya hizi qawaid hazijulishi kamwe suala la ***tadarruj***:

(a) Kwa sababu neno lake Mwenyezi Mungu (swt): ﴿فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ﴾ **"Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo"** [At-Taghaabun: 16] haina ufahamu wa kinyume, yaani haifahamiki kutokana na aya kwamba uchamungu hauamrishwi wakati inapokuwa hapana uwezo, bali ni kinyume na hivyo, aya inajulisha ulazima wa kutumia juhudi katika upatikani wa uchaji mungu na kujifunga na maamrisho ya Mwenyezi Mungu na makatazo yake. na imamu Twabari amedhihirisha hii maana katika tafsiri yake aliposema: "Neno lake Mwenyezi Mungu (swt): ﴿فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ﴾ **"Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo"** [At-Taghaabun: 16]: asema Mwenyezi Mungu (swt), na kuweni na tahadharini na Mwenyezi Mungu (swt) enyi waumini, na ogopeni mateso yake, na jiepusheni na adhabu yake kwa kutekeleza aliyowafaradhishia na kujiweka mbali na maasi yake, na kwa kutenda yanayowakaribisha kwake kadri ya uwezo wenu]… na amefanya vizuri ibn Ashur katika tafsir yake [at-Tahrir wa at-Tanwiir] pale alipoifafanua aya hii, kwa kusema:

***Endelea... UK 12***


Email: info@uqab.or.ke

فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَاسْمَعُوا وَأَطِيعُوا وَأَنْفِقُوا خَيْراً لِأَنْفُسِكُمْ وَمَنْ يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

**"Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo, na sikieni, na t'iini, na toeni, itakuwa kheri kwa nafsi zenu. Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio walio fanikiwa."** [At-Taghaabun: 16] herufi "faa" ni "faswiha" nayo ni kutanua yaliyotangulia, yaani ikiwa mumelijua hili basi mcheni Mwenyezi Mungu (swt) katika yanayopasa kutokana na taqwa... na kuondoshwa yanayohusiana na neno **(اتَّقُوا)** ni kwa kusudio la kueneza yanayohusiana na uchamungu katika hali zote zilizotajwa na nyenginezo. Kwa hiyo, maneno haya ni kama ukamilishaji, kwa sababu yaliyo ndani yake ni mapana zaidi kuliko yaliyo kabla yake. Na ilivyo "taqwa" ni kama tu mengine yaliyotajwa [ambapo] mtu mwenye taqwa anaweza kupatwa na mapungufu katika kutekeleza, kwa sababu ya pupa yake ya kutaka kuridhisha utashi wa nafsi yake katika hali nyingi ya hivyo vitu, ndio maana ikazidishwa kusisitizwa jambo la taqwa kwa kusema: **(مَا اسْتَطَعْتُمْ) "kwa kadri mnavyoweza"**. Na neno "maa" ni ya "maswdar" na "dhwarfu" yaani, [mcheni Mwenyezi Mungu] kwa mda wa uwezo wenu, ili [neno hilo] lienee zama zote, na ili lienee hali zote kutokana na kuenea kwake zama, na lienee pia uwezo wote. Hivyo basi wasijitenge na taqwa katika zama zozote, na zama zimefanywa ni dhwarfu ya uwezo ili wasizembee katika jambo lolote ambalo wanaliweza katika mambo waliyoamrishwa kuwa na taqwa nayo maadamu halitoki nje ya kipimo cha uwezo na kwenda kwenye kiwango cha mashaka/mazito...]" mwisho wa nukuu.

Kwa hiyo, aya inajulisha kwa uwazi kabisa juu ya ulazima wa kutumia juhudi katika kumcha Mwenyezi Mungu (swt), na kutoenda kombo na kuacha maamrisho yake na makatazo yake kwa kiasi anachoweza Muislamu. Wala haijulishi kwa namna yoyote ile juu ya tadarruj, yaani juu ya ufaaji wa kutekeleza hukmu za ukafiri kando na hukmu za sheria, bali [aya] inataka tujifunge na sheria kwa daraja ya juu zaidi ya kujifunga.

(b) Hadith tukufu ambayo imetumiwa kuwa dalili ya hizo qawaid zilizoashiriwa [huko mwanzo] ni kama ilivyopokewa na Bukhari katika Sahih yake kutoka kwa Abu Huraira, kutoka kwa Mtume (saw) akisema:

دَعُونِي مَا تَرَكْتُكُمْ إِنَّمَا هَلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ بِسُؤَالِهِمْ وَاخْتِلَافِهِمْ عَلَى أَنْبِيَائِهِمْ فَإِذَا نَهَيْتُكُمْ عَنْ شَيْءٍ فَاجْتَنِبُوهُ وَإِذَا أَمَرْتُكُمْ بِأَمْرٍ فَأْتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ

"[Niacheni madamu nimewaacha, kwani si kwa lengine waliangamia walokuwa kabla yenu kwa maswali yao na kutafautiana kwao na mitume wao. Hivyo basi, nitakapowakataza kitu kiepukeni, na nitakapowaamrisha jambo basi litekelezeni kwa kadri ya uwezo wenu]". Hii hadith yasema - kuhusu yalokatazwa - kwamba hakuna budi ila kujiepusha nayo, kwa hiyo yaloharamishwa ni wajib kujiweka mbali nayo moja kwa moja. Ama yaloamrishwa ndio ambayo yamefungamanishwa na uwezo. Na hapana shaka kwamba, kutekeleza hukmu za ukafiri kando na hukmu za Uislamu kwa madai ya tadarruj, hilo ni miongoni mwa mambo ambayo sheria imekataza tena kwa dalili za kukata. Kwani hakika amesema Mwenyezi Mungu (swt):

وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ

**"Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri."** [Al-Maidah: 44]

وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

**"Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu."** [Al-Maidah: 45]

وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

**"Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu."** [Al-Maidah: 45]

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْراً أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالاً مُبِيناً

**"Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na khiari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi."** [Al-Ahzab: 36]

Basi kwa hiyo, hiyo hadith haijulishi kwa namna yoyote ile juu ya kufaa kuzembea katika kuhukumu na sheria na [badala yake] kutabikisha hukmu za ukafiri kwa madai ya tadarruj. Kwa sababu, kuhukumu kwa sheria isiyokuwa aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu (swt) hilo ni miongoni mwa mambo yaliyoharamishwa, na ni katika makatazo ambayo hadith imewajibisha kujiepusha nayo.

Kwa misingi hiyo basi, bila shaka kutumia qaaidah hii kama dalili ya tadarruj katika kuzitabikishaa hukmu za sheria, huo ni utoaji dalili ulio batili ambao hoja kamwe haiwezi kusimama kwayo.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**05 Rabi ul-Akhir 1443 H**

**10/11/2021 M**


Email: info@uqab.or.ke